**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu kwa mawasiliano:-**

**Mkuu wa Shule: 0788266204**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0787307848**

**Matron/Patron: 0687220763**

**Shule ya Sekondari CHAMWINO,**

**S.L.P402, DODOMA.**

**Tarehe 25/04/2024.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO HALMASHAURI YA CHAMWINO MKOA DODOMA MWAKA 2024.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari **CHAMWINO** ipo umbali wa Kilometa 35 Mashariki mwa Mji wa DODOMA. Usafiri wa basi kutoka mjini **DODOMA** unapatikana katika kituo cha mabasi **MAKOLE.** Nauli ni Shilingi Elfu moja mia sita tu (1900/=). Ukishuka standi ya mabasi CHAMWINO, utapanda pikipiki au bajaji kuja shuleni kwa nauli ni shilingi elfu moja (1,000/=).
Muhula wa Masomo unaanza tarehe **01/07/2024**, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 29**/06/2024.** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **14/07/2024.**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Aje na Sare ya shule kama ifuatavyo:
   - Sketi mbili (02) rangi ya damu ya mzee kwa Wasichana (maruni-1). Ziwe na mshono wa linda box (mshono kama sketi za masista wa kikatoliki), ndefu usawa wa kifundo cha mguu (Enka).
   - kwa Wavulana ni Suruali mbili (02) rangi ya damu ya mzee (maruni-1) yenye marinda na isiwe ya kubana na ndefu inayofunika kiatu(isiwe don't touch my shoes) na Upana wa suruali kwa chini uwe inch 15 kwa chini.
   - Mashati mawili (02) rangi nyeupe – mikono mirefu.
   - Rangi ya Hijab (kijuba) kwa wanafunzi wa kiislamu ni rangi nyeupe, ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

ii. Sare ya Michezo ni T-shirt ya rangi ya bluu kwa wasichana na wavulana (Isiwe na maandishi yoyote).

iii. Viatu vya shule ni vyeusi (ngozi) vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.

iv. Soksi jozi mbili nyeupe za shule.

v. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.

vi. Sweta rangi damu ya mzee yenye V-shingoni kwaajili kipindi Cha baridi.

vii. Nguo za kushindia (shamba dress): Track suit rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana; sketi nyeusi kwa wasichana (ndefu usawa wa kifundo cha miguu); suruali nyeusi kwa wavulana (chini upana size inch 15).

viii. Tisheti (T-shirt) ya rangi ya blue yenye nembo ya shule kwa wavulana na wasichana inapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/= (Ili kuepusha kuwa na rangi tofauti). Sio ya lazima ila muhimu kwaajili ya mda usio wa vipindi.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari sita (06) - Quire 4.

ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika;

iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

v. Scientific Calculator;

vi. Godoro kwa kila mwanafunzi lenye ukubwa wa ft.2½ X 6

vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya LIGHTBLUE (BLUE BAHAR), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 ya rangi ya light blue.

viii. Nguo za ndani za kutosha;

ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;

xi. Vifaa vya kufanyia usafi:
   - Wanafunzi wanaosoma CBG: jembe 1 na mpini wake, mifagio 2 wa ndani na nje, dawa ya kusafishia choo (Aro) lita moja na fagio ya kukaushia Maji 1 (Plastic Floor Squeezer).

- Wanafunzi wanaosoma EGM: Kwanja 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje, dawa ya kusafishia choo (Aro) lita moja, na fagio ya kukaushia Maji 1 (Plastic Floor Squeezer).

### 2.3 Michango mbalimbali

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B: Malipo yote yafanyike kupitia akaunti ya shule ifuatayo;**
**Jina la akaunti**: Shule ya sekondari Chamwino E.K
**Akaunti namba**: 52810006441 NMB. Mwanafunzi aje na Bank pay-in-slip anaporipoti shuleni.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule : DOMINICK THOMAS SULLUMO**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO
S.L.P 402, DODOMA

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0788266204**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0787307848**
- **Mwandamizi Taaluma: 0718709797**
- **Mwandamizi Malezi: 0717199122**

…………………………………………………………………………………………………………

# ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

## A. GEOGRAPHY

1. Principle of physical geography, by F.J. Monkhouse
2. Geography; Integrated Approach, by D.Waugh
3. Practical geography for Africa, by J.M. Pritchard
4. General Geography in diagram, by R.B. Bunnert
5. Simplified physical geography (A-Level), by D.M. Mapunda
6. Statistical methods and the geographer, by S.Gregory
7. Certificate physical and human geography, by Goh Chang Leong

## B. BIOLOGY

1. New Understanding Biology, by Suzan Toole
2. Advanced biology principles and application, by C.J. Clegg and D.G. Mackean
3. Advanced biology, by Michael Kent
4. Biological Science, by D.J Taylor

## C. CHEMISTRY

1. Advanced Chemisrty Review, by William W. Davis (Mzumbe book shop project, 2004)
2. Physical chemistry by Delungu, et (Mzumbe book shop project, 1998)
3. Advanced Level Inorganic Chemistry part I and II.(Tanzania instate of education ,1995)
4. Organic Chemistry volume I. The Fundamental Princinples by I.L. Finar (Longman Ltd 1990) E:
5. Physical chemistry, by Ngaiza

## D. MATHEMATICS

1. Advanced Mathematics Vol. I, by ministry of education and vocational training
2. Advanced Mathematics, by shayo
3. Advanced Mathematics, by Tranter and Laube
4. Pure Mathematics vol. I and II , by Back House
5. Further Pure Mathematics, by Bostock and Chandler Rourke

## E. ECONOMICS

1. Introduction to positive economics, by Lipsey
2. Economics Planning and Economic Growth, by Brech R.
3. Contemporary economics theory and practice, by Wagura
4. Descriptive economics, 2nd Edition.

**SHULE YA SEKONDARI CHAMWINO**
**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI**
**HABARI ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la baba………………………………………………………………….……………………………
2. Kazi yake…………………………………………………………………………….……………………………
3. Jina kamili la mama…………………………………….. ………………………..…………………………..
4. Kazi yake…………………………………………………………………………….………………………….
5. Jina kamili la mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)…………………………...………………………
6. Kazi na Anwani ya Mlezi………………………………..…………………………….. …………………..
7. Nyumbani kwa baba (alipozaliwa mtoto)…………………………………..……………………………..

   Kijiji/Mtaa………………..…………………… Wilaya……………………………..………………………
   Kata………………………………………… Mkoa………………………………………………………
   Tarafa………………..……………………

8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba……………………..…… ……………..………………………………
9. Nambari ya simu………………………………………..…………….………………………………..
10. Anwani ya mahali pa kazi ya mama……………………………... ……………………………….....…
    ……………………………………………………………….…………………..……………………...
    Nambari ya simu……………………………..…………………….……………………………….
11. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo
    ……………………………………………….. ……………………………………………………………...

12. Mimi…………………………...(Baba/Mama/Mlezi wa mwanafunzi ……………………...............Nathibitisha kuwa taarifa zilizotolewa hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo, na kuwa nitawajibika kumhudumia gharama zote zitakazohitajika akiwa shuleni.

***NB: Nguo za nyumbani haziruhusiwi kuja nazo shuleni. Ni marufuku!!***

Tarehe **:**………………………………. Saini**:**………………………………

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To be completed by Medical Officer from a known Public Hospital or Health Centre in respect to all entrants.

Full name…………………………………………………………………… age…………………….………………

Sex…………………………………………………………………………...... year………………….……....................

1. Blood count (red and White)……………………………………………………………….............................
2. Urine analysis Test………………………………………………………………………………………………….
3. Syphilis Test…………………………………………………………………………………………......................
4. T.B. ……………………………………………………………………………………………………………………
5. Eye Test ………………………………………………………………………………………………………………..
6. Ears ……………………………………………………………………………………………………………………..
7. Spleen ………………………………………………………………………………………………………………….
8. Abdomen ………………………………………………………………………………………………………………

**N.B. Pregnancy test for girls is necessary.**

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical impairment, family disease, chronic infection etc.
……………………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

I certify that the above named individual is fit to pursue studies as stated above.

……………………………………… ……………………………….…………
Name and Designation Signature and Official stamp

……………………………………… ………………………………………………
**Station** **Date**

**NOTE:**

1. Medical officer during the course of this Examination please attend the individual according to any diagnosed case.
2. The dully-filled form must be handed to the Head of the school during registration week; under no circumstances should a student be registered without certification of his/her physical fitness.